**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI MENGELE

**APRILI, 2024**

**SHULE YA SEKONDARI MENGELE**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA MBARALI**
**SHULE YA SEKONDARI MENGELE**



**Namba za Simu**
**Mkuu wa Shule 0759817548**
**Makamu Mkuu wa Shule 0757243142**
**Matron 0763770854**

**Shule ya Sekondari Mengele**

**S.L.P 145**

**Tarehe 17/04/2024**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi**
**…………………………………………….**
**S.L.P ……………………………………**
**…………………………………………….**

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI MENGELE HALMASHAURI YA MBARALI MKOA WA MBEYA MWAKA 2024.**

1. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka **2024** na atasoma tahasusi ya **PCM/CBG/HKL**. Shule ni ya bweni na ni ya wasichana kwa kidato cha tano na cha sita. Hongera kwa kuchaguliwa kujiunga kidato cha tano katika shule ya sekondari Mengele.
2. **MAHALI SHULE ILIPO NA INAVYOWEZA KUFIKIKA**
   Shule ya Sekondari Mengele ipo umbali wa Kilometa 70 Kaskazini/Kusini/Mashariki/Magharibi mwa Mji wa **MBEYA**. Shule ya sekondari Mengele iko mji wa **Chimala wilaya ya Mbarali Mkoa wa Mbeya**, kama unatokea Mbeya mjini panda magari yanayokwenda **Rujewa** (**Pandia Nane Nane au Uyole**) utashukia **Chimala stendi Mpya** na chukua usafiri wa pikipiki hadi shuleni. Wanaotokea **Songea, Njombe, Dodoma, Dar es Salaam** n.k kuja Mbeya shuka Chimala stendi Mpya kisha chukua usafiri

wa pikipiki hadi shuleni. Nauli toka Mbeya mjini mpaka Chimala ni Tshs. 4,000/= na usafiri wa pikipiki kuja shuleni unapatikana stendi mpya kwa Tshs. 1,000/=

Muhula wa Masomo unaanza tarehe 01/07/2024, hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe 29/06/2024 Mwisho wa kuripoti ni tarehe itakayotajwa na wizara

## 1. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA:-

### 1.1 Sare za Shule

i. Sare ya shule hii ni sketi 02 rangi ya damu ya mzee ndefu za linda box mbele na nyuma kitambaa kigumu (Zifike kifundo cha unyayo) *kipande cha kitambaa kimeambatanishwa*

ii. Mashati mawili meupe ya mikono mirefu

iii. Rangi ya Hijab (kijuba) ni Nyeupe na Nusu kanzu tetroni isiyoangaza ifunike kifua cha mwanafunzi pia iwe ndefu kufikia kifundo cha mkono akisimama

iv. Sare ya Michezo ni Traksuti rangi ya Light Blue na Tshirt ya Taifa Stars na Raba.

v. Viatu vya shule ni vyeusi vya ngozi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi;

vi. Soksi jozi mbili nyeupe

vii. Sweta la shingo ya V rangi ya kijani kibichi

viii. Nguo za kushindia (*shamba dress*) gauni ya Dark Blue mshono solo kuanzia mbili ifike kwenye kifundo cha unyayo.

ix. Tai rangi ya damu ya mzee (ya kuning'inia) ziwe mbili

x. Tisheti ya kijivu yenye kola nyeusi (Form six) ya shule. Kwa mwanafunzi ambaye hata kuja nayo inapatikana shuleni kwa gharama ya Tshs. 15,000/=

### 1.2 MAHITAJI MENGINE MUHIMU AMBAYO MWANAFUNZI ANAPASWA KUJA NAYO SHULENI:-

i. Madaftari makubwa counter books **Q**3/**Q**4 zaidi ya kumi

ii. **Ream (A4)** ya Karatasi Mbili (2) kwa mwaka;

iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika

iv. Kwa wanafunzi wanaosoma **Biology** waje na Dissecting Kit. Kwa ambaye hata kuja nayo zitapatikana jirani na eneo la shule kwa **Tshs.45000/=**

v. Scientific Calculator (Kwa wanafunzi wa PCM na CBG)

vi. Kwa wanafunzi wa HKL waje na Advanced Learner's Dictionary (kwa matumizi yao darasani)

vii. Godoro futi **2½ x 6**, aje nalo

viii. Mashuka Jozi 2 (rangi ya pinki na bluu bahari), blanket 1, foronya za mito rangi ya pinki na bluu bahari 2, chandarua 1

ix. Nguo za ndani za kutosha

x. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe)

xi. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko
xii. Kwanja 1, jembe 1,panga 1, reki 1, fagio ya ndani (brashi ngumu 1), fagio ya ndani (brashi laini 1) na fagio ya chelewa 1
xiii. Laboratory coat rangi nyeupe 01, kwa wanafunzi wa masomo ya sayansi.
xiv. Sanduku la chuma na kufuri lake.
xv. Nakala ya Hati ya Matokeo (Result Slip) ya kidato cha Nne
xvi. Fomu ya afya (medical Examination Form) hakikisha imejazwa na kuthibitishwa na Daktari wa Hospitali ya serikali
xvii. Spring file moja (01)
xviii. Ni wajibu wa mzazi/mlezi kumkatia mtoto wake BIMA YA AFYA. Kwa ambae hana aje na Tsh. 50,400/= kwa ajili ya kukata BIMA YA AFYA kwa mwaka mmoja.

## 1.3 MICHANGO MBALIMBALI

**Shule za Bweni**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 2. | Tahadhari | 5,000/= |
| 3. | Nembo | 5,000/= |
| 4. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**N.B** Michango hii yote ilipwe kupitia akaunti ya shule
Jina la akaunti: **MENGELE SECONDARY SCHOOL**
Akaunti Na.: **61101100020 NMB**
Shuleni njoo na **PAY IN SLIP**

## 2. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 2.1 SHERIA NA KANUNI ZA SHULE

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;

v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote

ix. Kutunza mali za shule
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**2.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;

xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**3. VIAMBATISHO NA FOMU MUHIMU**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

**Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu**.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**Saini ya Mkuu wa Shule:** ……………………………………

**Jina la Mkuu wa Shule: PASKALIA E. MAGANGA**

**Mhuri wa Mkuu wa Shule:**

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule: 0759817548**
- **Makamu Mkuu wa Shule: 0757243142**
- **Mwandamizi Taaluma: 0765741686**
- **Mwandamizi Malezi: 0755188397**

**4. MAMBO MENGINE MUHIMU YANAYOPASWA KUKAMILISHWA NA KUWASILISHWA SHULENI NA MWANAFUNZI.**

**a) Medical Examination Form ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali**
**b) Fomu ya maelezo ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki migomo**
**c) Tamko la mzazi**

**NAKUTAKIA MASOMO MEMA**

**……………………………………….**
**PASKALIA . E. MAGANGA**
**MKUU WA SHULE**
**SHULE YA SEKONDARI MENGELE**

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**MINISTRY OF EDUCATION , SCIENCE, TECHNOLOGY AND VOCATIONAL TRAINING**
**MEDICAL EXAMINATION FORM**

MENGELE SECONDARY SCHOOL,
P.O BOX 145,
**CHIMALA-MBEYA.**
DATE .........../……../20…….

REF: NO.MSS/MEF/Vol.03
MEDICAL OFFICER,
**..…………………………………**
**…………………………………..**
**PART I**
**REF: FORM V**
**ENTRANT……………………………………………………………………**
AGE ……………………………… YEARS …………………… SEX …………………
Please examine the above named form one entrant as to his/her physical and mental fitness to persue secondary education at this school. The examination should include the following categories:-

1. Hemoglobin ……………………………………………………………………..
2. P.V Bleeding ……………………………………………………………………..
3. Sight …………………………………………………………………………….
4. Blood pressure ………………………………………………………………….
5. Urine analysis ……………………………………………………………………..
6. Stool examination ……………………………………………………………….
7. Pregnancy test ……………………………………………………………………..
8. Skin diseases …………………………………………………………………….
9. Leprosy ……………………………………………………………………………
10. Any deformity ……………………………………………………………………
11. Epilepsy ……………………………………………………………………………
12. Pulmonary tuberculosis ……………………………………………………..
13. Neurosis ……………………………………………………………………………
14. Venereal diseases ……………………………………………………………...
15. Eye test …………………………………………………………………………..
16. Ears ……………………………………………………………………………………
17. Chest …………………………………………………………………………………...
18. Spleen ………………………………………………………………………………….
19. Abdomen ……………………………………………………………………………
20. Other diseases eg: physical defects or impairments infectious/chronic/family diseases

…………………………………………………………………….

**PART II**

1. I have examine the above named form one Entrant and I certify that he/she is physical and mental fit/unfit to purse secondary education studies.
2. Other comments ………………………………………………………………….

Signature ………………………………………
Designation ……………………………………
Station ……………………………………….
Date ……………………………………………..
Official stamp ………………………………

**FOMU YA TAARIFA BINAFSI ZA MWANAFUNZI**

**SEHEMU A: TAARIFA YA MWANAFUNZI** (ijazwe na mwanafunzi)

JINA KAMILI (Kama kwenye result slip)
…………………………………………………………….
Tarehe ya kuzaliwa …../…./……. Kabila …………………… Dini ………………………
Tahasusi uliyochaguliwa ………………. Shule nitokayo ………………………………
Mahali niishipo ……………………. Mkoa ………………… Wilaya …………………
Anwani yako S.L.P ………………………………..

**SEHEMU B: TAARIFA ZA WAZAZI/WALEZI**

Jina la Baba/Mlezi ……………………………………… kazi yake …………………
Jina la Mama/Mlezi …………………………………….. kazi yake …………………
Wazazi/walezi wanaishi (wapi) …………………… pamoja/wametengana ……………..
Anwani ya mzazi/mlezi S.L.P …………………… SIMU……………………
Wakati wa likizo zote nitakuwa kwa (mtaje) …………………. Wapi ……………………
SIMU ………………………..
Nathibitisha kuwa taarifa nilizotoa hapo juu ni za kweli na sahihi

Sahihi ya Mwanafunzi …………………………. tarehe ………………………………

**KUKUBALI NAFASI** (Ijazwe na mwanafunzi mwenyewe)

Mimi ………………………………………………. Nimesoma maagizo na taratibu za Shule na Wizara kwa makini, na kuzielewa na nipo tayari kuzifuata. Hivyo nakubali nafasi niliyopewa na nitafika shuleni siku/tarehe husika kama zilivyopangwa.

Sahihi: …………………………. Tarehe ………………………………..

**KUTOSHIRIKI MGOMO/FUJO/MAKOSA YA JINAI**

(Ijazwe na mwanafunzi mwenyewe)

Mimi …………………………………………………… UMRI ………… Naahidi kwamba nitakuwa mwadilifu na mwaminifu, na kwamba sitashiriki wala kusababisha/kuchochea mgomo kwa namna yeyote ile, na nitatoa taarifa kwa utawala pale nitakapoona viashiria vya mgomo/fujo au uvunjifu wa amani shuleni.

Aidha naahidi kwamba hatua kali za kinidhamu zichukuliwe dhidi yangu ikiwa ni pamoja na kusimamishwa au kufukuzwa shule iwapo nitabainika kuwa nimeshiriki katika makosa yaliyoainishwa katika kifungu hiki.

JINA LA MWANAFUNZI …………………………………

SAHIHI ………………. TAREHE………………..

JINA LA MZAZI/MLEZI …………………………………

SAHIHI ………………. TAREHE……………..

**OFISI YA RAIS-TWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**A: TAMKO LA MWANAFUNZI KUKUBALI MAAGIZO NA KUFUATA SHERIA NA KANUNI ZOTE ZA SHULE**

(Ijazwe na mwanafunzi mwenyewe)

Mimi ……………………………….......................... niliyechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza mwaka ………………. Katika Shule ya Sekondari Mengele. Nimesoma na kuelewa sheria na kanuni zote zilizoandikwa. Ninakubali kujiunga na shule hii na ninaahidi kufuata sheria na kanuni zote za shule kwa wakati wote nikiwa mwanafunzi. Pia ninaahidi ya kwamba nitahudhuria shule siku zote za masomo na sitashiriki au kujihusisha katika migomo, fujo, makosa ya jinai na katika makosa yote yanayoweza kunifukuzisha shule.

**B:TAMKO LA MZAZI**

Mimi …………………………………. Mzazi/Mlezi wa ……………………………….. aliyechaguliwa kujiunga kidato cha kwanza mwaka ……………. Katika Shule ya Sekondari Mengele. Nimesoma na kuyaelewa maagizo, sheria na kanuni za shule.

Ninaahidi ya kwamba nitatekeleza maagizo yote ambayo yameainishwa katika fomu hii, ikiwa ni pamoja na mahitaji ya mwanafunzi wakati akijiunga na shule. Ninakubali/Sikubali kumtimizia mahitaji yake yote kama yalivyoanishwa na ninaahidi kuwa karibu naye ili kujua mwenendo wake kitaaluma , kinidhamu na pia kujua mahitaji yake.

**MAWASILIANO**

1. …………………………………………………
2. …………………………………………………

Mahusiano (weka √)

Baba ☐ Mama ☐ Bibi ☐ Mjomba ☐ kaka ☐ dada☐

Mengineyo (taja)…………

Nduguwanaoweza kumtembelea mwanafunzi picha, na namba zao za simu zimeorodheshwa hapa chini:

1. ........................................simu.....................................
2. ........................................simu....................................
3. ........................................simu....................................
4. ............................... .........simu.....................................

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Weka picha Zao hapa Kulingana na Namba hapo juu | 2 | Weka picha Zao hapa Kulingana na Namba hapo juu | 3 | Weka picha Zao hapa Kulingana na Namba hapo juu | 4 | Weka picha Zao hapa Kulingana na Namba hapo juu |

(I) **MAANDALIO YA JIONI:**

1. Kila mwanafunzi anatakiwa ahudhurie maandalio ya jioni siku zote za wiki(jumatatu hadi Jumapili saa 1:30 hadi saa 4:00 Usiku.)
2. Ili kufanikisha maandalio ya jioni, kila mwalimu wa somo atakuwa anatoa kazi na kuhakikisha kuwa kazi hizo zimefanywa.
3. Walimu wa zamu watakuwa wanasimamia maandalio ya joini kikamilifu.

(II) **KUWAHI:**

Kila mwanafunzi anatakiwa

1. Kuthamini muda
2. Kuwahi katika shughuli za shule kama zilivyopangwa katika ratiba ya kila siku
3. Kufika shuleni kwa tarehe zilizopangwa
4. Siku ya kufungua shule, atokapo likizo mwanao anatakiwa kuripoti tarehe na muda aliopangiwa, iwapo atachelewa kufika tarehe na saa aliyopangiwa hatapokelewa. Mzazi/mlezi aliyeandikishwa shuleni atalazimika kuja na mwanae shuleni ili apokelewe.

(III) **SARE YA SHULE**

Kila mwanafunzi anatakiwa kuwa katika sare ya shule wakati wote wa:-

1. Masomo darasani
2. Kutoka nje ya shule kwa shughuli za kishule
3. Baraza la shule
4. Kwenda hospitalini
5. Kwenda maandamanoni
6. Kazi za mikono (vazi la kazi)
7. Michezo
8. Kwenda kanisani au msikitini

(IV) **MIPAKA YA SHULE.**

Kila mwanafunzi azingatie mipaka ya shule kama ifuatavyo:-

1. Kutotoka nje ya mipaka ya shule bila kibali cha Mkuu wa shule
2. Kutotembelea sehemu zifuatazo isipokuwa kwa kibali maalum

(a) Chumba cha walimu (staffroom)
(b) Ofisi za shule
(c) Maabara
(d) Jikoni
(e) Nyumba za walimu na wafanyakazi wasio walimu.

**……………………………….**

**PASKALIA E. MAGANGA**
**MKUU WA SHULE**
**0759817548**

## ORODHA YA BAADHI YA VITABU VILIVYOPENDEKEZWA

| |
|---|
| **HISTORY**<br>1.Major Events in African History-Mwijage<br>2. The Political Economy, Imperialism-by Nabudere<br>3.Africa Since 1800-4th Edition-by Roland Oliver<br>. How Europe Underdeveloped Africa-W.Rodney<br>. Europe from 1815-by Peacock<br>. Major Issues in Africa History-ICD |
| **GEOGRAPHY**<br>1.General Geography in Diagrams-RB Bunnet<br>2.Regional Geography-Nyambari Nyangwine<br>3.Photography Interpretation and Elementary Surveying for Secondary Level New edition-Dura<br>4.Certificate Human and Economic Geography-Morgan and Leong Chang |
| **KISWAHILI**<br>***USHAIRI***<br>1.Kimbunga-G.Gora (Taasisi ya Uchunguzi Kiswahili-TUKI 1994<br>. Chungu Tanu-T.A Mvungi (Tanzania Publishing House)<br>. Mapenzi Bora-S.Robert (Mkuki na Nyota)2003<br>. Fungate ya Uhuru-M.S Khatibu(Macmillan and Aidan)<br>***RIWAYA***<br>1.Vuta nikuvute-Shafi(Mkuki na Nyota)1999<br>. Kufikirika-S.Robert(Mkuki na Nyota)2003<br>. Mfadhili-Hussein Tuwa(Mathew B/W and Stationaries) 2007<br>. Usiku Utakapokwisha-Mbunda Msokile(Macmillan and Aidan)2007<br>***TAMTHILIYA***<br>1.Morani-E.Mbogo (DUP)<br>. Kivuli kinaishi –Said Mohamed (Oxford University Press)<br>. Kwenye Ukino wa Thim-E.Hussein(University Press) |
| **GENERAL STUDIES**<br>1.General Studies(Communication Skills far A-level-M-Kadeghe<br>2. General Studies Notes (For A-Level V&VI)G. Mshiu and N. Nyangwine |

**ENGLISH LANGUAGE**

1.A complete Course for Form V&VI-Michael Kadeghe
. Teaching English as a Foreign Language-G-Broughton et.Al
. A grammar of Contemporary English-Quirk, et.Al
. Longman English Grammar-L.G Alexander
5.The real English Textbook For Advanced Level-By Michael Kadeghe Advanced English Dictionary

**NOVEL**

1.The Beautiful One Are Not Yet Born-A.K Amah
2.A Man of the PeopleC/.Achebe
3. Divine Providence-Mkuki na Nyota
4.BlackMamba-EAEP

**POETRY**

1.Selected Poems-Institute of Education
2.The Wonderful Surgeon and Other poems-Mkuki na Nyota

**CHEMISTRY**

1.Ramsden Chemistry
. Understanding Chemistry
. S.Chandi's Chemistry XI
. S.Chandi's Chemistry XII
5.Advanced Chemistry
Chemistry Review Paper I&2

**BIOLOGY**

1.Biological Science-DJ Taylor
2.Understanding Biology
. S.Chandi's BIOLOGY XI
. S.Chandi's BIOLOGY XII
4.Advanced Level Biology
5.Biology Review Paper 1&2

**BASIC APPLIED MATHEMATICS**

1.Basic Applied Mathematics F5
2. Basic Applied Mathematics F6

**PHYSICS**

CONTEMPORARY PHYSICS
UNDERSTANDING PHYSICS
ROGER'S PHYSICS
S. Chandi's PHYSICS XI & XII
NELKON PHYSICS
PHYSICS REVIEW PAPER 1&2

**BASIC MATHEMATICS**

TRANTA MATH'S
S.Chandi's MATHEMATICS XI & XII
PURE MATHEMATICS VOLUME 1&2
UNDERSTANDING MATHEMTICS
MATHEMATICS REVIEW PAPER 1&2

**Ni muhimu kwa mzazi kumnunulia mwanaobaadhi ya vitabu tajwa hapo juu kadiri utakavyoweza.**